

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
DIVISHENI YA KAZI
ILIYOKETI MOROGORO

MAOMBI YA MAREJE NA. 13 YA 2020

BAINA YA

**MOROGORO INTERNATIONAL SCHOOL.....MLETA MAOMBI
NA**

HONGO MANYANYA.....MJIBU MAOMBI

UAMUZI

Tarehe ya mwisho ya Amri: 20/05/2021

Tarehe ya Uamuzi: 27/05/2021

A. E. MWIPOPO, J.

Morogoro International School ambaye ni Mleta Maombi katika shauri hili la Marejeo ameleta maombi haya akiomba Mahakama irekebishe Uamuzi Mdogo wa Tume ya Usuluhishi uliotolewa katika mgogoro wa kikazi Na. CMA/MORO/156/2017 wa tarehe 17 Januari, 2020, na Mhe. Kayugwa, H. Msuluhishi. Hata hivyo kabla ya kusikiliza shauri la msingi la marejeo MJibu Maombi aitwaye Hongo Manyanya ambaye katika shauri hili alikuwa akiwakilishwa na Bw. Abdul Bwaga, Wakili, aliwasilisha taarifa ya pingamizi la awali na kuomba Mahakamani ilisikilize. Taarifa ya pingamizi ilikuwa na hoja mbili za kisheria kuhusu makosa ya kiapo cha Mleta Maombi. Hoja ya kwanza ni kuwa aya moja ya kiapo hicho haikuwa imethibitishwa na hoja

ya pili ni kuwa kiapo hicho kinachounga mkono shauri hili kilikuwa na makosa katika eneo la uthibitishaji wa kiapo mbele ya Ofisa wa Kiapo (jurat of attestation).

Wakili wa Mjibu Maombi aliamua kuachana na hoja yake ya kwanza ya kisheria na kuwasilisha kuhusu hoja yake ya pili kuwa kiapo cha Mleta Maombi kilikuwa batili kwa sababu mtiririko (format) wa eneo la uthibitishaji wa kiapo mbele ya Kamishna wa Kiapo lilikuwa kinyume cha sheria. Alieleza kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 na 10 cha Sheria ya Viapo na Matamko ya kisheria, Sura ya 366 ya Sheria, iliyorejewa mwaka 2019 (the Oath and Statute Declarations Act, Cap. 366, Revised Edition 2019) mtiririko wa kiapo unatakiwa uwe kama ilivyo katika fomu iliyo katika nyongeza ya sheria hiyo. Na alieleza kuwa sehemu hiyo ya uthibitisho huo unatakiwa kuwa kama ifuatavyo, nanukuu:-

*"This, Declaration is made and subscribed
by the said A. B. who is known to me
personally (or who has been identified to
me bythe latter being known
to me personally) this day of
(Signature, qualification and address of the person taking the declaration)"*

Wakili wa Mjibu Maombi alikuwa ana maoni kuwa pale sheria inapotumia neno "inatakiwa" (shall) basi ni lazima jambo hilo lifanyike. Na katika kifungu 10 cha Sheria hiyo, Sura ya 34, kinataka mtiririko wa eneo la

kuthibitisha kiapo kiwe kama kilivyo katika nyongeza ya sheria (schedule) na katika shauri hili kiapo cha Mleta Maombi hakijafuata mtiririko huo. Hivyo, Mtiririko wa eneo la uthibitishwaji na kiapo cha Mleta Maombi ni tofauti na kinyume na mtiririko uliopo katika sheria. Katika kuunga mkono hoja yake aliiomba Mahakama hii kurejea katika kesi ya **Changshun Liu** dhidi ya **Rebecca Daudi Mussa na Wenzake Wawili, maombi Na. 387 ya 2017**, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, iliyoketi Dar es Salaam, (haijaripotiwa), ambapo Mahakama iliona kuwa mtiririko uliotumika na Mleta Maombi ni tofauti na mtiririko unaoelezwa kifungu cha 5 na cha 10 cha Sheria hiyo na hivyo kufuta (struck out) maombi hayo kwa kuwa ni batili.

Aliendelea kueleza kuwa pale ambapo sheria imeweka wazi juu ya mtiririko unaopaswa kufuatwa basi kushindwa kufuata mtiririko huo hakukuweza kutibika (incurably defective). Msimamo huo uliotolewa katika kesi ya **Cheban Z. Mkinywa** dhidi ya **Pangea Minerals Ltd, Maombi ya Kazi Na. 36 la 2016**, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, iliyoketi Shinyanga (haijaripotiwa). Alieleza Mahakama ya Rufani ilikuwa na msimamo kama huo katika kesi ya **Puma Energy Tanzania Ltd dhidi ya Ruby Roadways (T) Ltd**, Rufaa ya Madai Na. 3 la 2018, Mahakama ya Rufani ya Tanzania, iliyoketi Dar es Salaam, ambapo Mahakama iliona kuwa kanuni ya lengo kuu (overriding objective or oxygen principle)

haiwezi kutumika bila kuzingatia taratibu za kisheria. Hivyo, uthibitisho wa kiapo cha Mleta Maombi hauko sawa na una makosa makubwa ambayo yanafanya shauri lote liwe batili. Na anaomba shauri hili lifutiliwe mbali (strike out).

Akijibu Mawasilisho ya Pingamizi, Profesa Siriatus Binamungu, wakili wa Mleta Maombi, alieleza mawasilisho yote ya Mjibu Maombi kuhusu pingamizi hayapo sahihi. Alieleza kuwa sheria ambayo inayoongoza uthibitisho wa kiapo sio Sheria ya Viapo na Matamko ya Kisheria, Sura ya 12 ya Sheria iliyorejewa mwaka 2019. Sheria hii inaongoza viapo (oath) vyta kimahakama na matamko ya kisheria (statutory declarations). Sehemu ya tatu ya sheria hiyo kuanzia kifungu cha 10-11 kinahusu matamko ya kisheria. Tafsiri ya maneno "matamko ya kisheria" ni maelezo rasmi, matamko au matangazo hususani ambayo yanatolewa katika hati. Hivyo, ni wazi kuwa sheria hii haitumiki katika uthibitisho wa kiapo.

Wakili wa Mleta Maombi alieleza sheria inayoongoza katika uthibitisho wa kiapo ni kifungu cha 8 cha Sheria ya Wathibitisha Viapo wa Umma na Kamishna wa Kiapo, Sura ya 12 ya Sheria kama ilivyorejewa mwaka 2019 (Notaries Public and Commissioners for Oath Act, Cap. 12 Revised Edition 2019). Alieleza kuwa sheria hiyo inaeleza kuwa uthibitisho wa kiapo unafanywa na Kamishna wa kiapo kwa kuingiza jina lake, sehemu na tarehe ya kiapo hicho kilipochokuliwa. Katika sheria hii msimamizi wa kiapo

ni Kamishna wa kiapo na sio afisa wa Mahakama kama ilivyo katika Sura ya 34 ya Sheria. Kuunga mkono maelezo yake alinukuu maamuzi ya Mahakama ya Rufaa katika kesi ya **DB Shopriya and Co. Ltd** dhidi ya **Bish International BV, (2002) EA 47;** kesi ya **M/S Bulk Distributing Ltd** dhidi ya **Happyness William Mollel, Maombi ya Madai Na. 64 ya 2008,** Mahakama ya Rufani ya Tanzania iliyoketi Arusha; na kesi ya **Darusi Gidahusi** dhidi ya **Jamhuri,** Maombi ya Jinai Na. 1 ya 2011, Mahakama ya Rufani ya Tanzania iliyoketi Arusha, ambapo katika kesi zote hizo Mahakama ya Rufani ilijielekeza katika Sura ya 12 ya Sheria kama sheria inayoongoza kiapo cha ushahidi (affidavit). Hivyo ni wazi kuwa sheria inayotumika katika viapo vya ushahidi (affidavits) ni Sheria ya Wathibitisha Viapo wa Umma na Kamishna wa Kiapo, Sura ya 12 ya Sheria kama ilivyorejewa mwaka 2019.

Akiendelea kuwasilisha, Wakili wa Mleta Maombi alieleza Mahakama hii inatakiwa ifuate maamuzi ya kisheria yaliyotolewa na Mahakama ya Rufani kama ilivyoamriwa katika kesi ya **Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania dhidi ya Kiwanda cha Uchapishaji cha Taifa, (1988) T.L.R.146.**

Aidha, Wakili wa Mleta Maombi alieleza uamuzi wa Mahakama hii katika kesi ya **Changashun Liu** iliyonukuliwa na Mjibu Maombi uliamuliwa kwa makosa. Akiendelea kuwasilisha Wakili alieleza Mjibu Maombi

anajaribu kuifanya mahakama iangalie sehemu tu ya nyongeza ya Sheria katika Sura ya 34 ya Sheria badala ya nyongeza yote. Ukisoma nyongeza hiyo kwa ujumla wake inaongelea matamko ya kisheria na sio viapo vya mashahidi. Alieleza kuwa pingamizi hili sio sahihi kwa kuwa sheria husika sio ya viapo vya mashahidi na anaomba pingamizi litupiliwe mbali (dismiss) na alipwe gharama za kusikilizwa kwa pingamizi hili.

Akifanya mawasilisho ya nyongeza (Rejoinder submission), Wakili wa Mjibu Maombi alieleza kuwa kesi zote zilizonukuliwa na Wakili wa Mleta Maombi zinaongelea maudhui ya uthibitisho wa kiapo na sio mtiririko wa kiapo. Hivyo kesi hizo zote hazihusiana na pingamizi hili hivyo naomba Mahakama isizingatie. Pingamizi ni kuhusu mtiririko wa uthibitisho wa kiapo (jurat of attestation) kuwa umetengenezwa na Mleta Maombi na sio maudhui yake. Sheria inayoongelea mtiririko wa eneo la utjibitisho wa kiapo ni Sheria ya Kiapo na Matamko ya Kisheria, Sura ya 12 ya Sheria.

Baada ya kusikiliza mawasilisho ya pande zote mbili hoja inayobishaniwa na inatakiwa iamuliwe na Mahakama hii iwapo kiapo cha Mleta Maombi ni batili kwa sababu eneo la uthibitisho wa kiapo kwa Kamishna wa kiapo ni kinyume cha sheria.

Katika pingamizi hili Mjibu Maombi ameeleza ya kwamba mtiririko wa kiapo cha Mleta Maombi upo kinyume na Sheria ya Kiapo na Matamko ya kisheria, Sura ya 34 ya Sheria iliyorejewa mwaka 2019 hususani kifungu

cha 10 na cha 5 cha sheria tajwa. Kwa upande mwingine, Mleta Maombi alieleza sheria inayoongoza katika uthibitisho wa kiapo ni kifungu cha 8 cha Sheria ya Wathibitisha Viapo vya Umma na Makamishna wa Kiapo, Sura ya 12 ya Sheria, Iliyorejewa mwaka 2019 na si Kifungu cha 5 na 10 cha Sheria ya Viapo na Matamko ya Kisheria.

Sheria ya Viapo na Matamko ya Kisheria, Sura ya 34 ya Sheria, imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ya sheria (Part I) inahusu vifungu vya awali (preliminary provisions) ambavyo ni kifungu cha 1 na 2. Sehemu ya pili (Part II) inahusu viapo vya Kimahakama (Judicial Oaths) ambayo inaanzia kifungu cha 3 hadi cha 10. Sehemu ya tatu ya sheria (Part III) inahusu Matamko ya Kisheria (Statutory Declarations) na inaanzia kifungu cha 10 hadi 11. Ukisoma jina lefu (long title) la Sheria linaeleza kuwa sheria hii inatumika kwa ajili ya usimamizi wa viapo na uthibitisho katika mwenendo wa kimahakama (judicial proceedings) na kwa ajili ya matamko ya kisheria. Kifungu cha 3 cha sheria hiyo kinaipa mamlaka Mahakama kusimamia viapo au uthibitisho wa mtu ye yote ambaye itaona ni sahihi kisheria kumhoji baada ya kiapo au uthibitisho. Hivyo ni wazi kuwa sheria hii inahusiana na kiapo kinachosimamiwa na Mahakama au Ofisa aliyeidhinishwa na Mahakama.

Mjibu Maombi aliwasilisha kuwa kifungu cha 5 na 10 cha Sheria Viapo na Matamko ya Kisheria, Sura ya 34 ya Sheria, kinataka mtiririko wa kiapo

uwe kama inavyoonekana katika fomu (form) iliyo katika nyongeza ya sheria hiyo. Nimesoma kifungu cha 5 cha sheria kinaleza kuwa viapo au uthibitisho unaofanywa chini ya sheria hii unatakiwa kuwa kama katika fomu iliyotengenezwa kwa kanuni zilizotengenezwa katika kifungu cha 8. Kifungu cha 8 chenyewe kunampa mamlaka Jaji Mkuu ya kutengeneza kanuni baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya kisheria. Kifungu cha 10 cha sheria hiyo kinaleza kuwa matamko ya kisheria yanatakiwa kuwa kama ilivyo fomu (form) iliyo katika nyongeza ya sheria. Hivyo ni wazi kuwa fomu (form) iliyo katika nyongeza ya sheria inahusu matamko ya kisheria na sio kiapo.

Kiapo cha ushahidi (affidavit) kinaongozwa na sheria mbalimbali ikiwa pamoja na Sheria ya Wathibitisha Viapo wa Umma na Makamishna wa Kiapo, Sura ya 12 ya Sheria iliyorejewa mwaka 2019. Kama alivyoeleza wakili wa Mleta Maombi, uthibitisho wa kiapo mbele ya Kamishna wa Kiapo (jurat of attestation) unaongozwa na kifungu cha 8 Sheria ya Wathibitisha Viapo wa Umma na Makamishna wa Kiapo, Sura ya 12 ya Sheria. Nakubaliana naye kuwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika maamuzi yake mbalimbali imekuwa ikieleza kuwa uthibitisho wa kiapo unatakiwa uwe kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria ya Wathibitisha Viapo vya Umma na Makamishna wa Kiapo, Sura ya 12. Kesi hizo ni pamoja na kesi ya **DB Shopriya and Co. Ltd** dhidi ya **Bish International BV**, kesi ya

M/S Bulk Distributing Ltd dhidi ya Happyness William Mollel, na kesi ya **Darusi Gidahusi** dhidi ya **Jamhuri** ambazo wakili wa Mleta Maombi alizinukuu.

Aidha, kifungu hicho cha 8 cha sheria hiyo hakijasema kuwa mtiririko wa eneo la uthibitisho wa kiapo unatakiwa uweje, bali kinataja mambo ya kuzingatiwa na kila Mthibitisha Kiapo cha Umma au Kamishna wa Kiapo wakati wa kuthibitisha kiapo. Mambo hayo ni jina la Mthibitisha Kiapo cha Umma au Kamishna wa Kiapo na aeleza kuwa anasema ukweli wa eneo na tarehe ambayo kiapo hicho kimetolewa mbele yake. Mahakama ya Rufaa ilikuwa na mtazamo kama huo wakati ikiongelea kiapo cha ushahidi (affidavit) katika kesi ya **Mkurugenzi wa Mashtaka** dhidi ya **Dodoli Kapufi na Patson Tusalile**, Maombi ya Jinai No. 11 of 2008, Mahakama ya Rufani iliyoketi Dar es Salaam (haijaripotiwa), ambapo Mahakama hiyo ilitamka kwamba, nanukuu:-

"The word "jurat" has its origin in the latin word "jurare" which meant "to swear". In its brevity a jurat is a certification added to an affidavit or deposition stating when, where and before what authority (whom) the affidavit was made. See, section 8 of the Notaries Public and Commissioner for Oaths Act, Cap 12 R.E. 2002. Such authority usually, a Notary Public and/or Commissioner for Oath, has to certify three matters, namely:- (i) that the person signing the document did so in his presence, (ii) that the signer appeared before him on the date and at the place indicated thereon, and (iii) that he administered an oath or affirmation to the signer, who swore to or affirmed the contents of the document."

Katika shauri tajwa hapo juu Mahakama ya Rufaa ilikuwa na mtazamo kuwa Uthibitisho wa Kiapo unatakiwa uoneshe kuwa mtu anayesaini kiapo amefanya hivyo mbele ya Kamishna wa Kiapo au Mthibitisha Viapo wa Umma; aliyesaini kiapo amefika mbele ya Kamishna wa viapo au mthibitisha kiapo mahali na tarehe iliyooneshwa; na kuwa Kamishna wa viapo au mthibitisha kiapo alisimamia kiapo au uthibitisho wa aliyesaini kiapo ambaye ameapa au kuthibitisha yaliyomo katika nyaraka hiyo. Na Mahakama ilieleza kuwa haya yanapatikana katika kifungu cha 8 cha Sheria ya Wathibitisha Viapo vya Umma na Makamishna wa Kiapo, Sura ya 12. Hivyo, ni wazi kuwa Sheria hii ndio inayotumika katika kuthibitisha kiapo.

Wakili wa Mjibu Maombi katika kuunga mkono mawasilisho yake alinukuu kesi ya **Changshun Liu** dhidi ya **Rebecca Daudi Mussa na Wenzake Wawili, maombi Na. 387 ya 2017**, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, iliyoketi Dar es Salaam, (haijaripotiwa), ambapo Mahakama hii iliona kuwa mtiririko uliotumika na Mleta Maombi ni tofauti na mtiririko unaoelezwa na kifungu cha 5 na cha 10 cha Sheria ya Viapo na Matamshi ya Kisheria, Sura ya 34 ya Sheria na hivyo kufuta (struck out) maombi hayo kwa kuwa ni batili. Hata hivyo, ni maoni yangu kuwa Mahakama katika kesi hiyo iliamua kimakosa kwa kuwa kifungu cha sheria

kilichonukuliwa hakihusiani na kiapo cha ushahidi bali kinahusu matamko ya kisheria.

Kwa sababu hiyo naona kuwa pingamizi halina msingi na nalitupilia mbali (dismiss). Shauri linaendelea na usikilizwaji kwa ustahili wake (on merits). Kwa kuwa shauri hili linahusu mgogoro wa kazi hakutaküwā Rā gharama ya uamuzi huu kwa upande wowote.



A. E. MWIPOPO
JAJI
27/05/2021